



Harusi kijijini



Tusome Early Literacy Programme

Harusi kijijini



Leo ni siku ya harusi ya Koki na Juma.

Wanakijiji wote wamekusanyika uwanjani kwa furaha tele.

Wapishi wameandaa vyakula vingi. Vyakula hivi ni kama vile: wali, nyama, samaki, sima na mboga. Wanakijiji pia wameleta maembe, nyanya, ndizi na sukumawiki kutoka sokoni.





Wazee kwa vijana wanafagia uwanja. Wanatumia fagio ili kuondoa takataka.

Bibi na bwana harusi wamevalia mavazi ya kupendeza.

Kiongozi anawaambia wanakijiji wapige foleni ili wapewe chakula.

Anawaambia ni muhimu kunawa mikono kabla ya kula.





Baada ya dakika chache, wanakijiji walianza kusukumana.

Wengine walikimbilia chakula na kukila bila kunawa mikono.

Kiongozi wa sherehe anawatuliza wanakijiji.
Anawaonya wasile bila kunawa mikono.
Anawaambia wasile maembe bila kuyaosha.






Baada ya harusi, wanakijiji waliokula bila kunawa mikono walianza kuumwa na tumbo.

Walipelekwa hospitalini kutibiwa.

Daktari alisema ni kwa sababu ya kula chakula bila kunawa mikono.

Anawaambia ni muhimu kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula chakula.



Maswali

1. Leo ni siku ya harusi ya nani?
2. Wapishi wameandaa vyakula vya aina gani?
3. Kwa nini wanakijiji waliumwa na tumbo?
4. Wazee na vijana wanafagia uwanja kwa kutumia nini?
5. Kwa nini wanakijiji wana furaha?

Harusi kijijini

Leo ni harusi ya Koki. Wanakijiji wanajitokeza kwa wingi. Lakini wanafanya makosa wakati wa kupakuliwa chakula - wanakula bila kunawa mikono!



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.